

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA




TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

NAOMBA KUTOA TAARIFA KWA UMMA WA WATANZANIA KUWA LEO TAREHE 06 JANUARI, 2022 NIMEANDIKA BARUA KWENDA KWA KATIBU MKUU WA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) KUJIUZULU NAFASI YA SPIKA WA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA. UAMUZI HUU NI BINAFSI NA HIARI NA NIMEUFANYA KWA KUZINGATIA NA KUJALI MASLAHI MAPANA ZAIDI YA TAIFA LANGU, SERIKALI NA CHAMA CHANGU CHA CCM.

PIA NAKALA YA BARUA YANGU HIYO YA KUJIUZULU NIMEIWASILISHA KWA KATIBU WA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA AJILI YA HATUA STAHILI KWA MUJIBU WA KATIBA YA NCHI NA SHERIA NYINGINE HUSIKA ILI KUWEZESHA MCHAKATO WA KUMPATA SPIKA MWINGINE UWEZE KUANZA.

NACHUKUA NAFASI HII KUTOA SHUKRANI ZANGU ZA DHATI KWA WABUNGE WENZANGU, MHE. RAIS SAMIA SULUHU HASSAN, SERIKALI KWA UJUMLA, WANANCHI WA JIMBO LANGU LA KONGWA NA WATANZANIA WOTE KWA USHIRIKIANO MKUBWA MLIONIPA KATIKA KIPINDI CHOTE NILIPOKUWA SPIKA WA BUNGE LETU TUKUFU.

MUNGU IBARIKI TANZANIA


JOB YUSTINO NDUGAI
06 JANUARI, 2022